



LEBA

Mpango mpya wa uthibitisho wa ujuzi kunufaisha vijana 40,000 **UK3**



MAZINGIRA

Serikali yazindua mpango wa miaka 10 wa kuokoa mnara mkubwa zaidi wa maji nchini **UK 15**

Septemba 23, 2025

MyGov.

www.gaa.go.ke

TATHMINI YAKO YA WIKI

TOLEO La. 13/2025-2026

Serikali kununua mahindi moja kwa moja kutoka kwa wakulima kuweka akiba

Waziri wa Kilimo na Ustawi wa Mifugo Mutahi Kagwe asema hatua hiyo itahakikisha sio tu usalama wa chakula kwa nchi, lakini pia itawapa wakulima soko tayari na la uhakika la mazao yao



Waziri wa Kilimo na Ustawi wa Mifugo, Mutahi Kagwe (Kulia), akikagua shamba la mahindi wakati wa awamu ya 57 ya Maonyesho ya Kilimo ya Kenya katika uwanja wa maonyesho wa Kabiru-ini Nyeri. Picha na Wangari Mwangi.



Takwimu za Wiki

70M

Idadi ya mifuko ambayo serikali itanunua moja kwa moja kutoka kwa wakulima mwaka huu ili kuongeza Hifadhi ya Kitaifa ya Chakula.

40,000

Idadi ya vijana watakatunukiwa vyeti na Mamlaka ya Kitaifa ya Mafunzo ya Viwanda (NITA) chini ya mpango wa uthibitisho yaani Recognition of Prior Learning (RPL).

4,096

Idadi ya nyumba za kisasa na za bei nafuu ambazo serikali inajenga katika Kaunti Ndogo ya Starehe.

700M

Kiasi ambacho serikali itatumia kuboresha Uwanja wa Gakoigo katika Eneo Bunge la Maragua kuwa uwanja wa kisasa wa viti 10,000.

6B

Gharama ya Huduma ya Reli kwa Wasafiri iliyozinduliwa hivi majuzi mjini Mombasa na Rais William Ruto.

10B

Thamani ya mradi wa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi ya Uvuvi wa Bahari ya Kenya (KEMFSED)



Find us also on;



Government Advertising Agency



@MyGovKe




@GAA_Kenya



https://gaa.go.ke

Contacts: mygovads@gaa.go.ke | editorial@gaa.go.ke | director@gaa.go.ke | (+254) 020 4920000/1



Serikali kuweka akiba ya chakula mavuno yakikaribia



Mwanamume akitembea karibu na shamba la mahindi linalonyauka Gatitu, kaunti ya Nyeri kwenye picha ya faili.

NA WANGARI MWANGI NA
DIANA ODIPO (KNA)

Serikali imetangaza mipango ya kuongeza akiba ya Taifa ya Chakula cha Dharura kwa kununua chakula moja kwa moja kutoka kwa wakulima huku nchi ikijiandaa kuvuna magunia mil-

ioni 70 ya mahindi mwaka huu. Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Mutahi Kagwe, alisema hatua hiyo haitahakikisha tu usalama wa chakula kitaifa bali pia itawapatia wakulima soko la uhakika na la kuaminika kwa mazao yao. “Usalama wa chakula nchini ume-kuwa thabiti, huku upatikanaji

ukiimarika na bei za vyakula vya msingi zikishuka. Tunapoelekea msimu wa mavuno makubwa, Serikali itajaza upya Akiba ya Taifa ya Chakula cha Dharura. Hii itahakikisha usalama wa chakula kwa taifa na kutoa soko la uhakika kwa wakulima,” alisema Kagwe. Mavuno ya mwaka huu, ambayo

Jedwili la takwimu na maelezo

Mavuno ya mwaka huu, yanayoelezwa kuwa ya kihistoria, yanazidi mavuno ya 2024 kwa magunia milioni 3 ya kilo 90. Mifuko milioni 70 inayotarajiwa ni zaidi ya mara mbili ya mifuko milioni 34.3 iliyovunwa mnamo 2022. Akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa toleo la 57 la Maonyesho ya Jumuiya ya Kilimo ya Kenya ya Kati katika Uwanja wa Maonyesho wa Kabiru-ini huko Nyeri, Kagwe alihusisha kuongezeka kwa uzalishaji na hali ya hewa nzuri na utoaji wa mbolea ya ruzuku na pembejeo nyingine na serikali kwa wakati. Alisema Serikali hadi sasa imeshatoa mifuko milioni 21.3 ya mbolea yenye thamani ya Sh53.25 bilioni kupitia Mpango wa Ruzuku ya Mbolea. Kwa msimu wa mvua ndefu wa 2025, baadhi ya mifuko milioni 6.9 ya mbolea ilisambazwa kwa wakulima. “Hii imepunguza bei ya mbolea kwa hadi asilimia 67 kwa kila gunia la kilo 50 na kuongeza uzalishaji wa bidhaa muhimu,” Kagwe alisema. Aidha alifichua kuwa mipango inaendelea ya kutoa mifuko milioni 12.5 ya mbolea ya ruzuku kwa misimu ya 2026 katika kata zote 1,450.

yameelezwa kuwa ya kihistoria, yanazidi mavuno ya mwaka 2024 kwa magunia milioni 3 yenye kilo 90 kila moja. Magunia milioni 70 yanayotarajiwa ni zaidi ya mara mbili ya magunia milioni 34.3 yaliyovunwa mwaka 2022. Akizungumza wakati wa ufunguzi rasmi wa Maonesho ya 57 ya Chama cha Kilimo cha Kenya Kanda ya Kati katika viwanja vya Kabiru-ini, Nyeri, Kagwe alihusisha ongezeko la uzalishaji na hali nzuri ya hewa pamoja na upatikanaji wa mbolea na pembejeo zingine kwa wakati kupitia mpango wa ruzuku wa serikali. Alisema Serikali hadi sasa imetoa magunia milioni 21.3 ya mbolea yenye thamani ya Sh53.25 bilioni kupitia Mpango wa Ruzuku ya Mbolea. Kwa msimu wa mvua ndefu wa mwaka 2025, takriban magunia milioni 6.9 ya mbolea yalisambazwa kwa wakulima. “Hii imepunguza bei ya mbolea kwa hadi asilimia 67 kwa kila gunia la kilo 50 na kuongeza uzalishaji wa mazao muhimu,” alisema Kagwe. Aidha, alifichua kuwa mipango inaendelea ya kusambaza magunia milioni 12.5 ya mbolea yenye ruzuku kwa misimu ya mwaka 2026 katika kata zote 1,450. Kagwe alisisitiza dhamira ya Serikali ya kufanya kilimo kuwa shughuli ya faida kwa wakulima kwa kutoa afueni ya masoko na ruzuku. Alibainisha kuwa kuanzishwa kwa Mfumo Jumuishi wa Taarifa za Usimamizi wa Kilimo Kenya (KIAMIS) kutarahisisha upatikanaji wa mbolea yenye ruzuku na pembejeo zingine kupitia mfumo wa vocha za kielektroniki wa serikali.



MASENO UNIVERSITY
OFFICE OF THE DEPUTY VICE-CHANCELLOR
(ADMINISTRATION, FINANCE AND DEVELOPMENT)



DECLARATION OF VACANCIES

In pursuit of its mission and mandate, the University wishes to invite applications from suitable qualified candidates to fill the positions indicated below:

EXTERNAL ADVERTISEMENT	
TEACHING POSITION - SCHOOL OF BUSINESS AND ECONOMICS	
1.	DEPARTMENT OF BUSINESS ADMINISTRATION
NON-TEACHING POSITIONS - OFFICE OF THE VICE-CHANCELLOR	
2.	DEPARTMENT OF LEGAL SERVICES
3.	DEPARTMENT OF INTERNAL AUDIT
4.	DEPARTMENT OF SECURITY SERVICES
5.	PROCUREMENT DEPARTMENT
OFFICE OF THE DEPUTY VICE CHANCELLOR, ADMINISTRATION, FINANCE & DEVELOPMENT	
6.	KISUMU HOTEL
7.	TRANSPORT DEPARTMENT

SCHOOL OF MEDICINE	
8.	DEPARTMENT OF HUMAN ANATOMY
9.	DEPARTMENT OF MIDWIFERY
TEACHING POSITIONS	
10.	DEPARTMENT OF FINANCE AND ACCOUNTING
SCHOOL OF PLANNING AND ARCHITECTURE	
11.	DEPARTMENT OF URBAN MAMANAGEMENT
NON-TEACHING POSITIONS - OFFICE OF THE VICE-CHANCELLOR	
12.	DEPARTMENT OF INTERNAL AUDIT
SCHOOL OF EDUCATION	
13.	DEPARTMENT OF SPECIAL NEEDS EDUCATION

Any canvassing will lead to automatic disqualification. Applicants should submit **ten (10) copies** of their applications on or before **13th October, 2025 at 5.00p.m.** Addressed to:

The Deputy Vice-Chancellor
Administration, Finance and Development
Maseno University
P.O. Box 333-40105 Maseno

Only shortlisted candidates will be contacted. Maseno University is an equal opportunity employer and therefore applicants of all gender, marginalized group and persons living with disability are encouraged to apply. Interested applicants should visit Maseno University Website www.maseno.ac.ke to view Specific vacant positions and detailed requirements.

ISO 9001:2015 CERTIFIED



THE EXECUTIVE OFFICE OF THE PRESIDENT
OFFICE OF THE PRIME CABINET SECRETARY AND
MINISTRY OF FOREIGN AND DIASPORA AFFAIRS
STATE DEPARTMENT FOR NATIONAL GOVERNMENT CO-ORDINATION

PUBLIC NOTICE

CALL FOR PUBLIC PARTICIPATION ON THE DRAFT RELIGIOUS ORGANIZATIONS POLICY, 2024 AND THE DRAFT RELIGIOUS ORGANIZATIONS BILL, 2024

The Presidential Taskforce on the Review of the Legal and Regulatory Framework Governing Religious Organizations in Kenya (the “**Taskforce**”) was constituted vide Kenya Gazette Notice Numbers 5661 of 5th May, 2023 and 6091 of 11th May, 2023. The Taskforce presented its Report to His Excellency the President on 30th July, 2024 and as part of its terms of reference, developed and recommended –

- a) the draft Religious Organizations Policy, 2024; and
- b) the draft Religious Organizations Bill, 2024.

The overall objective of these instruments is to provide a framework for regulation of religious organizations; to combat religious extremism and the abuse of the freedom of religion and connected purposes.

The drafts are available on the Office of the Prime Cabinet Secretary website through the weblink:
<https://www.primecs.go.ke/policies-bills-acts>

Following Cabinet's adoption of the Taskforce's Report on 29th July, 2025, the State Department for National Government Co-ordination, which is vested with the mandate of coordinating the implementation of the Taskforce's recommendations, hereby invites the public and all persons likely to be affected by the provisions of the documents above to submit written Memoranda on them. These should reach the undersigned through email address religiousorganizations@primecs.go.ke on or before **22nd October, 2025** using the template provided in the Office of the Prime Cabinet Secretary website through the weblink above.

Hard copies of the written Memoranda may be submitted to the Office of the Principal Secretary, State Department for National Government Co-ordination at the Office of the Prime Cabinet Secretary, Ground Floor, Kenya Railways Building, off Haile Selassie Avenue, Nairobi, and addressed as follows–

Hon. Ahmed Abdisalan Ibrahim
Principal Secretary
State Department for National Government Co-ordination
Kenya Railways Headquarters
P.O Box 30551-00100
Off Haile Selassie Avenue, NAIROBI

Public participation forums shall be announced in due course.

Hon. Ahmed Abdisalan Ibrahim
Principal Secretary
STATE DEPARTMENT FOR NATIONAL GOVERNMENT CO-ORDINATION

Programu mpya ya uthibitisho wa ujuzi kufaidi vijana 40,000 ikifadhiliwa na WB

NA JANE MASON
(PCO)

Mamlaka ya Kitaifa ya Mafunzo ya Viwanda (NITA) imezindua awamu ya uhamasishaji wa mpango wa Recognition of Prior Learning (RPL) unaolenga vijana zaidi ya 40,000 kote nchini. Mpango huu unakusudia kuendeleza ujuzi, kuongeza ajira na kupanua fursa kwa vijana walio katika mazingira magumu. Mchakato wa vyeti vya RPL unatekelezwa chini ya Mradi wa National Youth Opportunities Towards Advancement (NYOTA), mpango wa miaka mitano wa Serikali ya Kenya unaoungwa mkono na Benki ya Dunia. Mradi huu unalenga kuongeza ajira, kuinua kipato, na kukuza akiba miongoni mwa vijana wa Kenya. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NITA, Theresa Wasike, alisema kuwa awamu ya uhamasishaji ni muhimu kwa kuwaandaa wanufaika kabla ya kuanza mchakato wa uthibitishaji. "Awamu ya uhamasishaji ni muhimu sana kwa sababu

itawasaidia wanufaika wa RPL kuelewa mchakato mzima wanapoanza safari yao kuelekea mustakabali bora," alisema wakati wa kikao cha mtandaoni na waratibu wa mpango huo ngazi ya mashinani siku ya Alhamisi. Hadi sasa, NITA imeendelea shughuli za uhamasishaji katika kaunti 20, ikiwemo Samburu, Garissa na Trans-Nzoia, huku kaunti zilizobakia zikitarajiwa kufikiwa katika awamu zinazofuata. Kwa mujibu wa Mtaalamu wa RPL, Solomon Eyanae, ambaye aliongoza kikao katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi cha Maralal, Samburu, awamu ya uhamasishaji itafungua njia kwa uchunguzi na uwasilishaji wa ushahidi. Katika hatua hii, vijana wataongozwa na wataalamu wa NITA kubaini ujuzi wao na kuwasilisha uthibitisho kama vile picha, vielelezo vya kazi, ushuhuda au video. Wanufaika baadaye watapitia mtihani wa mwisho wa tathmini, ambao unaweza kujumuishia mitihani ya vitendo, maandishi au maswali ya



mdomo ili kuthibitisha umahiri wao. Watakao-faulu watatunukiwa cheti cha kitaifa kinachotambuliwa na NITA kama ushahidi wa ujuzi wao. Mbali na vyeti vya RPL, NITA pia itafanya yafuatayo: Kuwapima na kuwatu-

nuku vyeti vijana waliopata ujuzi wa kiufundi kupitia mafunzo kwa vitendo (internship). Kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa ili kuhakikisha yanakidhi viwango vya sekta. Kuwaendeleza walimu

mafundi bingwa (Master Craftsmen) wapa-tao 4,000 ili kuimarisha mbinu zao za ufundishaji. Kusaidia katika kuandaa viwango vya mafunzo ya ufundi stadi (apprenticeship standards) katika sekta mpya ikiwemo

uchumi wa kidijitali, buluu, kijani, kijivu na ubunifu. Mratibu wa Mradi wa NITA, Joseph Kinuthia, alisisitiza kuwa juhudi hizi zitawawezesha vijana wa Kenya kupata ujuzi unaohitajika sokoni na kufungua njia mpya za ajira endelevu.



MINISTRY OF LABOUR & SOCIAL PROTECTION

State Department for Labour and Skills Development
Directorate of Occupational Safety and Health Services

PUBLIC PARTICIPATION ON THE REVIEW OF LEGAL NOTICE NO. 50 OF 2022, THE OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH (FEES CHARGED FOR OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH SERVICES) REGULATIONS

The Ministry of Labour and Social Protection through the Directorate of Occupational Safety and Health Services invites the public to provide input on the proposed reviewed Occupational Safety and Health (Fees Charged for Occupational Safety and Health Services) Regulations, 2025. The review is pursuant to section 127(1) of the Occupational Safety and Health (OSH) Act 2007.

The objective of the review is to expand the scope of OSH services beyond those listed in the 2022 regulations and align the associated charges with present-day valuation standards.

All stakeholders including the Tripartite Partners, Occupiers, Workers and the members of the public are hereby requested to submit their views on the draft regulations. The draft Regulations 2025 can be downloaded from our websites www.labour.go.ke, and www.doshmis.go.ke.

Comments in the format of the template provided below, should be addressed to the Secretary, Occupational Safety and Health and submitted through email address doshdept@labour.go.ke and copy doshdept@yahoo.com not later than 5.00pm on 13th October, 2025.

Regulation No.	Clause Details	Suggested amendment	Justification/Comment

This call for submissions will last for 21 days from **23rd September to 13th October, 2025.**

Dr. Musa Nyandusi, OGW
Secretary, Occupational Safety and Health
P.O. Box 34120-00100
NAIROBI



PHARMACY AND POISONS BOARD

PUBLIC NOTICE

NOTICE FOR THE NOVEMBER 2025 PROFESSIONAL EXAMS

The Pharmacy and Poisons Board will conduct the Pre-registration Exams (Stage I & II) and Enrolment exams (Level I & II) on **November 17th, 18th & 19th, 2025.**

The exams will be administered **online** in the respective **examination centres.**

Each candidate should:

- Make an application using the **PPB online services portal**. The application deadline will be **31st October, 2025.**
- Select their preferred examination centre. The exam centres are subject to change, and candidates must regularly check the portal before the exam for any changes.
- Obtain a suitable computer device with internet access, that can be fully charged and store power to run for at least 3 hours.

Rehearsals will be conducted on **Monday, 17th November**, at the respective centres and are mandatory. Mock exams will be conducted to familiarize candidates with the **PPB online examinations portal**. The dates for the mock exams will be communicated in due course. The mock exams will be done at home.

Candidates with disabilities or health issues that may affect their ability to sit for **online exams** must immediately notify the Board in writing, together with supporting medical evidence.

Any feedback or queries can be sent by e-mail to training@ppb.go.ke.

CHIEF EXECUTIVE OFFICER



Waziri aonya kaunti zilizochelewa Taveta ikizindua mpango wa nishati

NA ARNOLD LINGA MASILA
(KNA)

Waziri wa Nishati na Madini, Opiyo Wandayi, amezihimiza kaunti ambazo bado zinasuasua kuharakisha uandaji wa mipango yao ya nishati, akisisitiza kuwa nchi haiwezi kusubiri bila kikomo. Kauli yake ilijiri wakati ambapo Kaunti ya Taita Taveta ikawa ya saba kati ya kaunti 47 kuzindua rasmi mpango wake wa kina wa nishati. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Nishati wa Kaunti ya Taita Taveta katika Voi Wildlife Lodge, Wandayi alibainisha kuwa kaunti kadhaa bado zinacheleweka mipango ya nishati, akisisitiza kwamba maendeleo ya taifa hayawezi kuzuiliwa na wanaosuasua. “Hii ni onyo kwa kaunti ambazo bado ziko nyuma. Sitaki kutaja majina, lakini kuna kaunti kadhaa bado hazijaandaa mipango yao ya nishati,” Wandayi alisema. “Nchi haiwezi kusubiri milele. Kenya inataka kusonga mbele, na Taita Taveta imeonyesha njia.” Waziri huyo alisisitiza kuwa nishati ina nafasi ya msingi na kimkakati katika ndoto za maendeleo ya Kenya, akiielezea kama injini kuu ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kimuundo. Alieleza kuwa safari ya Kenya kuelekea maendeleo jumuishi na endelevu inahitaji nishati ya kuaminika, ya ushindani, nafuu na safi ili kufanikisha malengo ya kitaifa ya maendeleo. Wandayi alieleza kuhusu mageuzi makubwa ya sekta ya nishati nchini, akibainisha kuwa kiwango cha upatikanaji



Waziri wa Nishati na Petroli Opiyo Wandayi Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Kawi wa Kaunti ya Taita Taveta mjini Voi.

wa umeme kitaifa kimepanda kwa kasi kutoka takriban asilimia 29 mwaka 2013 hadi zaidi ya asilimia 95 kwa sasa. Alionyesha uongozi wa Kenya katika ukuzaji wa nishati mbadala, akisema kuwa vyanzo vya nishati mbadala kwa sasa vinachangia takriban asilimia 82 ya jumla ya uwezo

wa kuzalisha umeme uliosimikwa nchini na asilimia 93 ya matumizi halisi ya nishati. “Kenya inaongoza bara la Afrika kwa uwezo wa kuzalisha nishati ya jotoardhi na kushika nafasi ya sita duniani,” Wandayi alisema, akiongeza kuwa nchi pia inajivunia mtandao mpana wa usafirishaji umeme

wa kilomita 9,484, ukiwemo miunganisho ya kikanda inayoweza biashara ya umeme kuvuka mipaka.

Hata hivyo, Waziri huyo alikiri kuwa changamoto bado zipo. Alieleza kuwa takriban asilimia 25 ya Wakenya bado hawana upatikanaji wa umeme, wengi wao wakiwa maeneo ya vijijini. La kusikitisha zaidi, alibainisha kuwa zaidi ya asilimia 65.5 ya kaya bado zinategemea kuni na mkaa wa kienyeji kupikia, jambo linalochangia ukataji miti, hatari za kiafya na uharibifu wa mazingira. Ili kukabili changamoto hizi, Wandayi alieleza mikakati muhimu ikiwa ni pamoja na kupanua na kuboresha miundombinu ya nishati, kuhamasisha matumizi yenye tija ya nishati, na kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa taasisi za kijamii na umma. Alisisitiza haja ya kuwepo kwa mifumo ya udhibiti yenye usawa ili kuhakikisha uthabiti na uhakika wa mtandao wa umeme, na kuibadilisha sekta ya umeme kuwa nguvu shindani katika masoko ya ndani na kikanda. Waziri huyo alisisitiza umuhimu wa mipango ya nishati ya kaunti katika kufanikisha malengo ya kitaifa, akieleza kuwa kan-

Hatuwezi kuunda Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Nishati bila kuleta mipango ya kaunti husika

uni mpya za Mpango Jumuishi wa Nishati wa Kitaifa (INEP) zilizochapishwa zimetengeneza mfumo wa upangaji wa kina. “Hatutaweza kuan- daa Mpango Jumuishi wa Nishati wa Kitaifa bila kuhusisha mipango ya nishati ya kaunti husika,” alisema. Alisifu dhamira ya kaunti hiyo ya kupanga kwa ushirikishi, akibainisha kuwa mpango huo umejumuisha maoni kutoka kwa kaunti ndogo zote nne za Voi, Mwatate, Wandanyi na Taveta, na hivyo kuhakikisha umuhimu wa kijamii na ushiriki wa jamii. Waziri huyo alifichua kuwa wizara yake kwa sasa inasaidia kaunti zingine 17 ambazo ziko hatua za mbele kuan- daa mipango yao ya nishati, akionyesha matumaini kuwa kaunti zote 47 hatimaye zitakamilisha mchakato huo. “Kila mtu ataingia kwenye mchakato huu hatimaye. Mtazamo wetu ni kuharakisha mchakato huu,” alihimiza. Akikiri mchango wa washirika wa maendeleo, Wandayi alimtaja hasa Umoja wa Ulaya kupitia Mradi wa Usaidizi wa Kiufundi Endelevu na Mradi wa Mfuko wa Hali ya Hewa wa Kijani (Climate Friendly Cooking) unaofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Ujerumani. Alishukuru ushirikiano na msaada wa kiufundi uliotolewa kwa kaunti katika kuan- daa mipango yao ya nishati. Waziri huyo alisisitiza kuwa dhamira ya sekta hiyo ya kutoa nishati ya kuaminika, shindani na endelevu itaunda ajira, kuongeza kipato na kusaidia ukuaji wa uchumi wenye nguvu. Alieleza mipango ya mifumo ya fedha endelevu na bunifu pamoja na mikakati ya kupunguza hatari ili kuvutia uwekezaji na kuchochea ushiriki shindani wa sekta binafsi.

Serikali kuvutia vijana katika utumishi wa umma

NA LAMECH WILLY
(PCO)

Serikali inaunda mikakati sya kuongeza idadi ya vijana katika utumishi wa umma, kwa lengo la kuondoa dhana ya kizamani kwamba sekta hiyo inatawaliwa na maafisa wakongwe. Katibu wa Wizar ya Utumishi wa Umma na Maendeleo ya Rasilimali Watu, Dkt. Jane Imbunya, alisisitiza tena dhamira ya serikali ya kuunda nafasi zaidi kwa ajili ya vijana. Akizungumza katika Jumba la Harambee wakati wa mkutano wa majadiliano na vijana kutoka maeneo mbalimbali nchini, Dkt. Imbunya alieleza ajenda ya serikali ya kupanua fursa kwa vijana kitaifa na kimataifa. “Tumewaalika vijana hapa leo kwa sababu wako katikati ya ajenda yetu. Kila mwaka idadi kubwa yao wanahitimu vyuoni na kubaki bila ajira. Siamini kwamba vijana wanapaswa kuandaliwa tu kwa ajili

ya kesho—wao ndio nguvu ya leo,” alisema Dkt. Imbunya. Aliongeza kuwa majadiliano hayo yalijikita katika maeneo mahsusi, yakiwemo maswali kuhusu utumishi wa umma na majibu kutoka kwa wataalamu wa kiufundi wa Idara ya Utumishi wa Umma na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Katibu huyo pia aliwahakikishia vijana kwamba serikali inafanya kazi ya kuunda njia zaidi za ajira, hususan kupitia mpango wa Digital Superhighway, ambao unatarajiwa kufungua nafasi nyingi za ajira. Ili kuziba pengo la ukosefu wa uzoefu miongoni mwa wahitimu wapya, serikali kwa ushirikiano na Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) imekuwa ikiendesha Mpango wa Mafunzo kwa Vijana katika Utumishi wa Umma (PSIP) tangu mwaka 2018. Mpango huu unatoa nafasi ya mwaka mmoja isiyoweza kurejelewa katika Wizara, Idara, Mashirika ya Serikali na Vyuo Vi-



Katibu wa Utumishi wa Umma na Maendeleo ya Rasilimali Watu Dkt. Jane Imbunya akitangamana na vijana kutoka kote nchini wakati wa mkutano wa meza ya mduara katika Harambee House.

kuu vya Umma, na tayari ume- faidisha zaidi ya vijana 30,000. “PSIP umeundwa kusaidia wahitimu kupata ujuzi wa vitendo na uzoefu wa kazi, hivyo kuongeza uwezo wao wa kujiriwa,” alieleza Dkt. Imbunya.

Siamini kwamba vijana wanapaswa kujiandaa kwa ajili ya kesho pekee—ndio nguvu ya leo

Aidha, nafasi nyingine za mafunzo ya kazi pia zimeanzishwa, zikiwemo Mpango wa Mafunzo wa Mamlaka ya Mapato Kenya (KRA), na Mpango wa Mafunzo wa Mamlaka ya ICT, unaowapa wahitimu wa ICT mafunzo ya uongozi na fursa za kujenga mitandao ya kitaaluma. Mikakati hii yote inalenga kuwaandaa na kuwapa vijana ujuzi wa kuchukua nafasi mbalimbali katika utumishi wa umma. Akijibu hoja zilizotolewa na vijana, Mkurugenzi wa Sera za Usimamizi wa Rasilimali Watu, Martin Situma, alithibitisha kwamba serikali inaunda sera mpya za kupanua nafasi za mafunzo ya kazi. “Tunafanya kazi ya kuongeza idadi ya nafasi za mafunzo kutoka 5,000 hadi 30,000 kupitia ushirikiano na sekta binafsi. Mfumo unaundwa kwa kushirikiana na wadau ili kufanya jambo hili kuwa halisi,” alisema Situma. Vijana waliokuwa washiriki walipokea kwa furaha dhamira ya serikali, wakisema kwamba mikakati hiyo itasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza ukosefu wa ajira na kuhakikisha uwakilishi zaidi wa vijana katika utumishi wa umma.

Waendesha baiskeli wazunguka EAC kuinua uelewa wa hali ya hewa

NA ANNE KANGERO (KNA)

Waendesha baiskeli kumi na wawili kutoka nchi tano za Afrika Mashariki wako katika dhamira ya kukamilisha safari ya kilomita 6,000 kote katika eneo hilo kwa siku 55, wakihusisha jamii kuhusu hatua za

kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, usalama wa chakula, na mshikamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Waendesha baiskeli hao, waliotoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ni sehemu ya Great Africa Cycling



Waendesha Baiskeli kutoka Great Africa Cycling Safari wakiagwa na Naibu Kamishna wa Kaunti ya Machakos David Rotich katika ofisi ya Kamishna.

Safari, mpango wa kila mwaka unaoandaliwa kwa ushirikiano na Kings Cycling Mind, kundi linaloongozwa na wana-harakati wa mazingira kutoka Kenya. Kampeni hii inalenga kukuza uhi-fadhi wa mazingira kwa kupanda miti ya matunda katika shule, vijiji, na maeneo kame katika eneo lote la Afrika Mashariki. Wakizungumza katika Shule ya Upili ya Machakos, ambako walipanda miche ya matunda, kiongozi wa timu, John

Baptist, alisema kuwa safari hiyo ilianza Kampala mapema Agosti 2025 na tayari wamepitia Rwanda, Burundi, Kongo na Tanzania kabla ya kuingia Kenya kupitia mpaka wa Namanga. "Hii ni mwaka wetu wa nane tangu tulipoanza nchini Uganda mwaka 2017. Mabadiliko ya tabianchi ni janga linalohitaji hatua za haraka, na safari hii ya baiskeli ni njia mojawapo ya kuelimisha na kuunganisha jamii katika EAC," alisema Baptist.

Serikali yaongeza nyumba za bei nafuu katika mtaa wa Starehe jijini Nairobi

NA BERNADETTE KHADULI (KNA)

Serikali inajenga jumla ya nyumba 4,096 za kisasa na za bei nafuu chini ya Mpango wa Nyumba za Bei Nafuu (AHP) katika Kaunti Ndogo ya Starehe, ambazo wanunuzi wataweza kupata kupitia jukwaa la Boma Yangu kwa bei zilizopunguzwa. Nyumba hizo zimegawanywa katika makundi matatu: vitengo 2,364 vya bei nafuu, vitengo 400 vya soko la kawaida, na vitengo 1,062 vya kijamii kwa wananchi wa kipato cha chini. Nyumba hizo zitakuwa kati ya chumba kimoja hadi vitatu, ambapo chumba kimoja kitauzwa kwa bei ya chini ya Shilingi 640,000. Akilihutubia jopo la Kamati ya Utekelezaji na Uratibu wa Miradi ya Serikali Kuu katika Kanda na Kaunti (NGD-RICMC/CICMC) ikiongozwa na Kamishna wa Kanda ya Nairobi, Gilbert Kitiyo, wakati wa ziara ya ukaguzi wa kazi zinazoendelea, Meneja Mkuu wa Starehe kutoka kampuni ya Gulf Cap Limited, Caroline Njeru, alisema nyumba hizo zinajengwa katika ardhi ya serikali yenye ukubwa wa ekari 22, ili-yogawanywa katika sehemu mbili, na zitakuwa na majengo 21, kila moja likiwa na ghorofa 13. Mradi huu wa nyumba za kisasa pia utajumuisha huduma za kijamii kama vile jengo la maegesho, kituo cha kibiashara, kituo cha malezi ya awali ya watoto, kituo cha jamii, kituo cha polisi na zahanati kwa ajili ya kuhudumia jamii ya jirani. "Tayari tumekamilisha nyumba za mfano kwa vitengo vya aina ya soko, na kufikia mwaka 2027 tutakuwa tumekamilisha mradi mzima," aliahidi Bi. Njeru.



- Kamati ya Utekelezaji na Usimamizi wa Kanda/Kaunti (NGD-RICMC/CICMC) ikiongozwa na Kamishna wa Mkoa wa Nairobi Gilbert Kitiyo ikitembelea mradi wa nyumba za bei nafuu wa Starehe, Nairobi.**
- Afisa Mkuu Mtendaji (CEO) Gulf Cap Limited Chris Ochieng aonyesha timu ya Kamati ya Uratibu na Usimamizi ya Utekelezaji wa Serikali ya Kitaifa ya Nairobi-Mkoa/Kaunti (NGD-RICMC/CICMC) ikiongozwa na Kamishna wa Mkoa wa Nairobi Gilbert Kitiyo kupitia ramani ya mchoro wa nyumba za bei nafuu za Starehe. picha: Bonface Malinda/KNA**

Eneo hilo la ekari 22 awali lilikuwa na takriban nyumba 360 za serikali za zamani, pamoja na makazi holela (mtaa wa mabanda wa Matopeni) uliokuwa na familia 770 ambazo zilikuwa zimejenga makazi yasiyo rasmi. Nyumba zote zisizopangwa zimebomolewa ili kupisha nyumba hizi za kisasa. Njeru alisema mradi huo umezalisha ajira kwa angalau wakazi 250 kutoka eneo hilo, na akaongeza kuwa mradi unavyoendelea, ajira zaidi zitabuka ikiwemo kwa mafundi wa Jua Kali kutoka Kamukunji, Ngong

na Kariobangi ambao watapewa kandarasi ya kutengeneza milango na madirisha ya chuma kwa ajili ya nyumba hizo. Kamishna wa Kanda alimwambia mkandarasi kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa mafanikio na ndani ya muda uliokubalika. RC Kitiyo aliwahimiza watumishi wa umma wanaohudumu katika Kaunti na ambao wizarao zinahusiana na utekelezaji wa AHP kushirikiana na kuunga mkono miradi inayotekelezwa katika maeneo yao ili kuhakikisha mafanikio yake.



THE INFORMATION AND COMMUNICATIONS TECHNOLOGY AUTHORITY

Kenya Digital Economy Acceleration Project (KDEAP)
ICTA-Program Implementation Unit

REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (Consulting Services – Firms Selection)

Country:	Kenya
Name of Project:	Kenya Digital Economy Acceleration Project (KDEAP)
Project No.:	P170941
Credit No:	7289-KE and 7290-KE
Assignment Title:	CONSULTING SERVICES FOR KENYA REVENUE AUTHORITY'S E-INVOICING PLATFORM SIMPLIFICATION, ENHANCEMENT AND REDESIGN, AND SUPERVISION OF IMPLEMENTATION
Contract No.:	KE-ICTA-500783-CS-QCBS

- The Government of Kenya has received financing from the World Bank towards the cost of the Kenya Digital Economy Acceleration Project (KDEAP) and intends to apply part of the proceeds for consulting services.
- The consulting services ("the Services") include Consulting Services for Kenya Revenue Authority's E-Invoicing Platform Simplification, Enhancement and Redesign, And Supervision of Implementation. The assignment is expected to take Eighteen (18) calendar months from the date of contract commencement.
- The detailed Terms of Reference (TOR) for the assignment can be found at the following websites: www.icta.go.ke/tenders and www.tenders.go.ke or can be obtained at the address given below.
- The Information and Communications Technology Authority through the Program Implementation Unit (PIU) now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are:
 - Core business and years in business:** The firm must be registered/incorporated as a consulting firm with core business in the field of ICT Systems and solutions Development and Delivery or related field for a minimum of five (5) years
 - Relevant experience:** The firm shall demonstrate as having successfully executed and completed at least two (2) assignments of a similar nature both in scope and complexity in a similar operating environment in the last four (4) years. Details of these assignments, including client names and addresses, scope, contract value, contract duration and year/period of assignment, must be provided
 - Technical and managerial capability of the consulting firm:** The firm shall demonstrate as having the requisite technical capacity and managerial capacity to undertake the assignment in the submitted company profile(s).

Key Experts will not be evaluated at the shortlisting stage.

- The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" First Published July 2016 and Revised Fifth Edition September 2023 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.
- Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected.
- A Consulting firm will be selected in accordance with the Quality and Cost Based Selection (QCBS) method set out in the Procurement Regulations.
- Further information can be obtained at the address below during the following office hours 0900 and 1600 hours from Monday to Friday excluding lunch hour (1300 to 1400hours) East African Time (EAT) and public holidays.
- Expression of interest must be delivered in written form by **8th October 2025 at 1000hours EAT** - using one of the following modalities: (i) deposit in the tender box located on 12th Floor, Telposta Towers, Kenyatta Avenue in Nairobi, Kenya or (ii) send by email to: procurement@icta.go.ke and quote the Assignment title and Contract No. in the subject row. For expressions of interest that will be deposited at the tender box, the packages should be clearly marked **Consulting Services for Kenya Revenue Authority's E-Invoicing Platform Simplification, Enhancement and Redesign, And Supervision of Implementation; Contract No. KE-ICTA-500783-CS-QCBS**

Address:

Ag. Chief Executive Officer,
The Information and Communications Technology Authority,
P.O Box 27150, Kenyatta Avenue
00100, Nairobi, Kenya.

Tel.: (+254) 20 667 6999 / E-mail: info@icta.go.ke / procurement@icta.go.ke
Attn: Deputy Director, Supply Chain Management

Uwanja wa Gakoigo Maragua kupigwa jeki kwa Sh700M

NA BERNARD MUNYAO
(KNA)

Serikali itatumia Shilingi milioni 700 kubadilisha Uwanja wa Gakoigo ulioko katika Eneo Bunge la Maragua kuwa uwanja wa kisasa wenye uwezo wa kuketi watu 10,000. Akizungumza wakati wa ziara yake katika uwanja huo, Katibu Mkuu wa Michezo, Elijah Mwangi, alisema uwanja huo am-

bao umetumika na jamii tangu enzi za kabla ya uhuru, umechelewa sana kufanyiwa ukarabati. “Kwa miaka mingi, Gakoigo umeandaa mikutano mingi ya hadhara, vikao vya jamii, maonyesho ya kilimo (ASK), na mashindano ya michezo. Lakini muda na uharibifu umeuacha ukiwa wa kizamani na umechakaa. Sasa uwanja huo unakaribia kupata uhai mpya,” alisema Mwangi.



Katibu wa Michezo Elijah Mwangi akikagua ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Mirira, Kiharu, Murang'a.

Alifafanua kuwa mradi huo, ambao ni utekelezaji wa agizo la Rais, utajumuisha barabara ya kukimbia yenye njia nane, uwanja wa mpira

wa miguu wa kiwango cha kimataifa, vyumba vya kubadilishia nguo vya kisa, pamoja na vifaa vya usalama vilivyoboreshwa. “Mara tu utakapo kami-

lika, uwanja huo utakuwa na uwezo wa kuandaa mashindano ya kitaifa na kimataifa, na hivyo kuifanya Maragua ijujikane katika ramani ya michezo,” aliongeza. Katibu huyo alibainisha pia kuwa uwekezaji huo ni sehemu ya mkakati mpana wa serikali wa kubadilisha sekta ya michezo nchini. “Kwa makusudi tumewekeza rasilimali katika miundombinu itakayounda nafasi za ajira, kuchezea ukuaji wa uchumi, na kuzipa nguvu jamii. Muhimu zaidi, viwanja kama Gakoigo vitatusaidia kubaini, kulea na kukuza vipaji vya vijana,” alisema Mwangi. Aidha, alitangaza kuwa

serikali pia inafanya mipango ya kujenga uwanja mwingine wa kisasa katika Uwanja wa Mumbi mjini Murang'a. Katibu huyo, ambaye pia alikagua ujenzi unaendelea wa Chuo cha Michezo cha Mirira kilichoko Wadi ya Mbiri katika Eneo Bunge la Kiharu, ambacho kwa sasa kimekamilika kwa asilimia 30, alisema fedha tayari zimetengwa katika bajeti ya sasa ili kuharakisha ujenzi wa viwanja hivyo. Kuhusu Chuo cha Michezo cha Mirira, Mwangi alibainisha kuwa ni miogoni mwa vyuo 37 vinavyojengwa kote nchini chini ya Awamu ya Kwanza kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.7.

Viongozi washinikiza sera za kisayansi kuokoa chemchemi ya Mto Mara



Viongozi wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mkutano huo. Picha na Chris Mahandara

NA CHRIS MAHANDARA
(KNA)

Viongozi wa kikanda wametoa wito wa mabadiliko makubwa katika usimamizi wa Bonde la Mto Mara, wakazitaka serikali kuanzisha sera zinazotegemea utafiti wa kisayansi, kushirikiana katika hatua za mipakani, na kuimarisha jitihada za uhifadhi zinazoongozwa na jamii ili kulinda rasilimali hiyo ya pamoja. Wito huo ulitolewa wakati wa Mkutano wa Kisayansi wa Siku ya 14 ya Mara, uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere (MNUAT), Wilaya ya Butiama, Tanzania. Mkutano huo, ambao ni sehemu ya maadhimisho ya kila mwaka ya Siku ya Mara, uliwaleta pamoja viongozi, wanasayansi, watunga sera na wawakilishi wa jamii ili kujadili njia za kuhifadhi mfumo wa ikolojia wa Mto Mara,

ambao unakabiliwa na vitisho vikubwa. Dkt. Masinde Bwire, Katibu Mtendaji wa Tume ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC), alisisitiza jukumu la utafiti katika kuamua mustakabali wa mto huo, unaouendeleza Hifadhi ya Maasai Mara nchini Kenya na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti nchini Tanzania. Alibainisha kuwa mkutano huo ulipokea zaidi ya machapisho 100 ya kitaaluma, ambapo 36 yalichaguliwa baada ya mchujo mkali ikiwa ishara ya kujitolea kwa ukanda huo katika uhifadhi unaotegemea ushahidi. “Sayansi, kama viongozi, lazima ijengeke juu ya kusudi, jamii, na maendeleo ya taifa,” Dkt. Bwire aliwaambia washiriki. “Uboara wa tafiti zilizowasilishwa mwaka huu unatupa matumaini kwamba hatua zinazofuata za uhifadhi zitaongozwa na ushahidi, si kwa kubahatisha.” Katibu Mkuu wa Wizara

ya Maji na Umwagiliaji wa Tanzania, Mhandisi Mwajuma Waziri, ambaye alifungua rasmi mkutano huo, alisifu ushirikiano kati ya Kenya na Tanzania katika kulinda mto wa kimipaka. Aliwataka wadau wasizishie maneno pekee, bali kuongeza uelewa, kuwawezesha wananchi wa eneo hilo, kuchapisha matokeo ya kisayansi, na kutumia maarifa ya asili. “Mkutano huo unajenga daraja kati ya mawazo, sera, na utekelezaji,” alisema. Afisa Mkuu wa Idara ya Maji, Mazingira na Malaria katika Kaunti ya Narok, William Tumanka Ololoigero, alifichua kuwa serikali ya kaunti na ile ya kitaifa zimekamilisha kazi ya kufunga uzio wa umeme kuzunguka msitu wa Mara na eneo la vyanzo vya maji ili kukomesha uvamizi. Alisema pia kuna miradi ya upandaji miti inayoendelea kurejesha mandhari yaliyoharibika.



REPUBLIC OF KENYA



Investing in rural people

THE NATIONAL TREASURY AND ECONOMIC PLANNING

RURAL KENYA FINANCIAL INCLUSION FACILITY

GENERAL PROCUREMENT NOTICE

Government:	Republic of Kenya
Project/ procuring entity:	The National Treasury, Rural Kenya Financial Inclusion Facility (RK-FINFA) Project
GPN Version:	2.0
GPN publication date:	23 rd September 2025

The Government of the Republic of Kenya has received financing from the International Fund for Agricultural Development (IFAD) towards the cost of the National Treasury Rural Kenya Financial Inclusion Facility (RK-FINFA) Project and intends to apply part of the financing to payments for contracts for goods, works, and services.

The procurement program for the 2025-2026 period will include the following:

Procurement for 2025-2026 Estimated value – USD 800,000
Procurement of goods to include:
Not Applicable
Procurement of works to include:
Not Applicable
Procurement of consulting services to include:
• Fiduciary Review
• Procurement of medical cover for project staff
Procurement of non-consulting services to include:
• Framework for Conference Services

The contract for goods, works, and services will be implemented in accordance with the principles, rules, and procedures set out in the current versions of the IFAD Project Procurement Guidelines and the IFAD Procurement Handbook.

Specific procurement notices for contracts to be tendered under the competitive bidding procedures will be announced as they become available on selected portals, in local newspapers, and other media outlets as appropriate.

Interested eligible bidders and consultants who wish to be included on the mailing list to receive a copy of advertisement, or those requiring additional information, should send an email to the rkfinfa@treasury.go.ke using the subject line “ GPN 2.0 for the National Rural Kenya Financial Inclusion Facility (RK-FINFA) Project and indicating which of the procurement items they are interested in.

THE PROJECT COORDINATOR
RURAL KENYA FINANCIAL INCLUSION FACILITY (RK-FINFA) PROJECT
FOR: PRINCIPAL SECRETARY, NATIONAL TREASURY



Kiunga kipya cha reli kurahisisha trafiki, kupunguza msongamano



Muonekano wa mbele wa kituo kipya cha reli cha Mombasa kinachounganisha Miritini, Changamwe Magharibi, Changamwe Mashariki, Shimanzi na Mombasa Central Business District (CBD).

NA SADIK HASSAN AND JOYCE HADRINE (KNA)

Ni mwanzo mpya kwa usafiri wa mijini wa Mombasa kufuatia uzinduzi wa Huduma ya Reli ya Abiria yenye thamani ya Sh bilioni 6, miaka 130 tangu Reli ya Kenya-Uganda ianze kufanya kazi katika Kituo cha Reli cha kihistoria cha Mombasa, kinachojulikana kwa jina maarufu la "Kilomita Sifuri." Uzinduzi wa Reli ya Kiunganishi ya SGR-CBD yenye thamani ya Sh bilioni 6 ni hatua kubwa ya kihistoria. Mradi huu, ulioanza mwaka 2022, unatarajiwa kusanafirisha abiria 4,000 kila siku, kupunguza msongamano wa magari barabarani na kuhakikisha usafiri unaoendelea bila vikwazo. Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Rais William Ruto, akiwa ameanadamana na Naibu Rais Prof. Ki-

thure Kindiki, Mawaziri Davis Chirchir (Barabara na Usafiri), Hassan Joho (Uchumi wa Buluu, Madini na Masuala ya Baharini), Salim Mvurya (Michezo), na Katibu wa Utoaji Huduma za Usafiri Mohamed Daghar. Mradi huu, unaoelezewa kama wa mageuzi makubwa, unatarajiwa kubadilisha jinsi watu wanavyosafiri kuingia na kutoka jijini la bandari. Unatoa suluhu kwa msongamano wa barabara na ucheleweshaji ambao wasafiri wa Madaraka Express wamekuwa wakivumilia kwa muda mrefu. Huduma ya usafiri wa reli ya abiria itatoa safari ya haraka, yenye uhakika na salama. Itapunguza msongamano wa barabarani, ajali, na muda wa safari kati ya Mombasa na kituo cha SGR cha Miritini. Treni pia itasaidia kupunguza

msongamano katika Kisiwa cha Mombasa, kwa kusimama katika vituo vya Miritini, Changamwe Magharibi, Changamwe Mashariki na Shimanzi. Waziri wa Barabara na Usafiri, Davis Chirchir, alisisitiza kwamba serikali inaweza makusudi kwenye miundombinu ya barabara, reli na bahari—sio kama miradi ya pekee, bali kama nguzo zinazoshiriki—ana katika mfumo jumuiishi wa kitaifa wa usafiri. Alieleza kuwa huduma ya reli ya abiria ya hatua ya mwisho itaunda fursa kwa wafanyabiashara wadogo, kupunguza gharama za usafiri na muda wa safari, kuingiza pesa kwenye masoko ya wenyeji, na kukuza maendeleo jumuiishi. "Huduma ya Reli ya Abiria ya Mombasa ni kauli ya wazi ya kile ambacho sera jumuiishi ya usafiri inaweza kufanikisha. Inahusu kuun-

ganisha miji, kuongeza tija, na kujenga mitandao ya kisasa ambapo kila aina ya usafiri inakamilisha nyingine," alisema Chirchir. "Kwa kuimarisha usafiri wa reli Pwani, hatuboresha tu usafiri wa mijini bali pia tunaimarisha nafasi ya Kenya kama kitovu cha kanda cha biashara, utalii na usafirishaji. Huduma hii itaunga mkono moja kwa moja shughuli za bandari, kupunguza utegemezi wa usafiri wa barabara na msongamano," aliongeza. Aidha, Waziri alibainisha kuwa reli ya abiria ni salama, na ni huduma ya kijamii inayotolewa

kwa ruzuku kubwa ili kuwahimiza wasafiri kuitumia. Chirchir pia alithibitisha dhamira ya Wizara kujenga mfumo wa usafiri jumuiishi unaowahudumia Wakenya wote na kuiweka nchi kama kitovu cha usafiri. Waziri alithibitisha kuwa Sh bilioni 2.1 za fidia kwa Watu Walioathiriwa na Mradi (PAPs) kandokando ya reli ya abiria ya Mombasa tayari zimetolewa kwa Tume ya Ardhi ya Kitaifa, na akawahimiza kuharakisha ulipaji kwa PAPs hao. Aidha, alifichua kuwa mkandarasi anaandaa mpango wa kupendezesha njia ya reli.



THE INFORMATION AND COMMUNICATIONS TECHNOLOGY AUTHORITY

Kenya Digital Economy Acceleration Project (KDEAP)
ICTA-Program Implementation Unit

REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST
(Consulting Services – Individual Selection)

Country:	Kenya
Name of Project:	KENYA DIGITAL ECONOMY ACCELERATION PROJECT (KDEAP)
Project No.:	P170941
Credit No:	7289-KE & 7290-KE
Assignment Title:	SENIOR TECHNICAL OFFICER (PROCESSES & STANDARDS)
Contract No.:	KE-ICTA-500817-CS-INDV

- This Request for Expression of Interest follows the General Procurement Notice for this project that appeared in MyGov Newspaper on 24th October, 2023.
- The Government of Kenya has received financing from the World Bank towards the cost of the Kenya Digital Economy Acceleration Project (KDEAP) and intends to apply part of the proceeds for consulting services.
- The consulting services ("Services") include digital infrastructure specialist (individual consultant). The assignment is expected to be completed within thirty-six (36) calendar months from the date of contract commencement.
- The detailed Terms of Reference (TOR) for the assignment can be found at the following website: www.icta.go.ke / www.tenders.go.ke
- The Information and Communications Technology Authority (the "Client") through the Project Implementation Unit (PIU) of Kenya Digital Economy Acceleration Project (KDEAP) now invites eligible individual consultants ("Consultants") to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services (attach detailed curriculum vitae (CV), copies of documentary evidence of academic qualifications, professional qualifications, and registration/licensing with professional bodies (as applicable). The shortlisting criteria is:
 - At least a Bachelors' degree in any of the following fields: Information Technology, Computer Science, Telecommunication, Electrical and Electronics Engineering or equivalent qualification from a recognized institution from a recognized institution, with a higher degree an advantage;
 - A minimum of six (6) years of general experience in the ICT or technology sector.
 - A minimum of two (2) year of specific experience in ICT standards and processes within a technology-focused organization
 - Professional Certification in any of the following: CCNA, CISA, OCP, ITIL, COBIT, CISSP, CCSA, or equivalent.
- The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" First Published July 2016 and Revised Fifth Edition September 2023, ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.
- A Consultant will be selected in accordance with the Selection of Individual Consultants method set out in the Procurement Regulations.
- Further information can be obtained at the address below from 0900 to 1700 hours East African Time (EAT) from Monday to Friday excluding lunch hour (1300 to 1400hours EAT) and public holidays.
- Expressions of interest must be delivered in a written form to the address below by **8th October 2025, at 1000hours EAT**, using one of the following modalities: (i) deposit in the tender box located on 12th Floor, Telposta Towers, Kenyatta Avenue in Nairobi, Kenya or (ii) send by email to: procurement@ict.go.ke and quote the Assignment title and Contract No. in the subject row. For expressions of interest that will be deposited at the tender box, the packages should be clearly marked **SENIOR TECHNICAL OFFICER (PROCESSES & STANDARDS)**; Contract No. **KE-ICTA-500817-CS-INDV**.

Address:

Chief Executive Officer,
The Information and Communications Technology Authority,
P.O Box 27150, Kenyatta Avenue
00100, Nairobi, Kenya.
Tel.: (+254) 20 667 6999
E-mail: info@ict.go.ke / procurement@ict.go.ke
Attn: Deputy Director, Supply Chain Management

P.O Box 61130-00200,
Nairobi, Kenya
Tel. (020) 499 7000
Mobile: 0709 781 000/0730 997 000
Email: supply-chain@integrity.go.ke



INTEGRITY CENTRE
Valley Rd/Jakaya Kikwete Rd Junction
23rd September, 2025

TENDER INVITATION

The Ethics and Anti-Corruption Commission (EACC) invites sealed tenders from eligible bidders for the listed tenders.

No.	EGP TENDER REF:	EGP NO	CLOSING DATE	ELIGIBILITY
1.	EACC/183/0007/2025-2026 SUPPLY, DELIVERY OF AUXILIARY GENERATOR SITE VISIT ON 26th SEPTEMBER, 2025 FROM 1000 HRS	TENDER ID:14	6 th OCTOBER, 2025	PWD
2.	EACC/183/0010/2025-2026 PROVISION OF GROUP LIFE INSURANCE COVER	TENDER ID:18	7 th OCTOBER, 2025	OPEN
3.	EACC/183/0012/2025-2026 SUPPLY, DELIVERY AND INSTALLATION OF WIRELESS NETWORK ACCESS POINTS	TENDER ID:22	7 th OCTOBER, 2025	OPEN
4.	EACC/183/0016/2025-2026 SUPPLY, DELIVERY AND INSTALLATION OF NETWORK SWITCHES	TENDER ID:34	9 th OCTOBER, 2025	OPEN
5.	EACC/183/0017/2025-2026 SUPPLY, DELIVERY AND INSTALLATION OF STORAGE AREA NETWORK DRIVES	TENDER ID:37	9 th OCTOBER, 2025	OPEN
6.	EACC/183/0018/2025-2026 PROVISION OF ANNUAL MAINTENANCE FOR SERVERS AND STORAGE	TENDER ID:39	9 th OCTOBER, 2025	OPEN

All Interested suppliers are required to register on the Electronic Government Procurement System (e-GPs) vide <https://egpkenya.go.ke> to be able to access the tenders.

Completed tenders shall be submitted through the e-GP System as per the requirements contained in the Tender Document.

Further, interested bidders are encouraged to keep visiting the platform from time to time to appraise themselves on any procurement opportunities.

The Commission wishes to inform the bidders that this tender notice supersedes the tender advert placed on the Government Advertising Agency (GAA) dated **Tuesday, 9th September, 2025**.

SECRETARY/CHIEF EXECUTIVE OFFICER
ETHICS AND ANTI-CORRUPTION COMMISSION.



Kenya inaunga mkono juhudi za kimataifa za kulinda 'ozone layer'



Waziri wa Mazingira Dkt. Deborah Barasa atembelea vibanda vya maonyesho wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ozoni Duniani katika bustani ya John Michuki Memorial, Nairobi. Picha: Joseph Ng'ang'a

NA NAIF RASHID AND MARY NDANU (KNA)

Kenya imethibitisha upya dhamira yake ya kulinda tabaka la ozoni na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wakati dunia ikiadhimisha miaka 40 tangu kupitishwa kwa Mkataba wa Vienna wa Kulinda Tabaka la Ozoni. Akizungumza wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Ozone Duniani katika Bustani ya Ukumbusho wa John Michuki jijini Nairobi, Waziri wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misititu, Dkt. Deborah Barasa, alisema kuwa ahadi za Kenya chini ya Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal zinaonyesha azma ya nchi kulinda mazingira pamoja na afya ya umma. Dkt. Barasa alieleza tabaka la ozoni kama “ngao isiyoonekana” ya binadamu inayolinda maisha duniani dhidi ya miale hatari ya urujuanimmo, akisisitiza kwamba kulilinda kunahitaji mshikamano wa kimataifa pamoja na hatua za kitaifa na kijamii. “Dhamira yetu ni rahisi lakini ya maana—kufanya vizazi vijavyo viishi bila madhara ya miale ya urujuanimmo na gesi zinazoongeza joto duniani. Ndiyo maana Kenya imekubali Marekebisho ya Ki-

gali ambayo yanashughulikia hidroflorokaboni, gesi zenye nguvu za chafu zenye uwezo mkubwa wa kusababisha ongezeko la joto duniani,” alisema Dkt. Barasa. Alibainisha kuwa Kenya ilijiunga na Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal mwaka 1988 na tangu wakati huo imeridhia marekebisho yote matano. Alisisitiza kuwa mpango wa utekezaji wa HFC wa Kigali wa Kenya, uliopitishwa katika kikao cha 93 cha Kamati Tendaji ya Mfuko wa Kimataifa, unatoa mfumo wa kupunguza hatua kwa hatua matumizi ya hidroflorokaboni kulingana na malengo ya kimataifa. Waziri huyo alitangaza pia kuwa Kenya imetengeneza Mpango wa Kitaifa wa Hatua za Ubaridi unaolenga kuhakikisha kaya, hospitali, kilimo na biashara zinapata huduma salama, nafuu na endelevu za ubaridi. Katibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Mhandisi Festus Ng'eno, kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu wa Mazingira, Dkt. Selly Kimosop, alisema Kenya imepiga hatua kubwa katika kutimiza wajibu wake chini ya Itifaki ya Montreal na Marekebisho ya Kigali.

Kenya yazindua mpango wa kilimo mseto ili kufikia lengo la miti 15b

NA NAIF RASHID NA LUCY MWENDE (KNA)

Kenya imechukua hatua kubwa katika ajenda yake ya uhi-fadhi wa mazingira kwa kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo cha Misitu 2025-2035 na Mfumo wa Ufuatiliaji wa Urejeshaji wa Mandhari na Mifumo Ikolojia wa Kenya 2025. Hatua hii inatarajiwa kuharakisha kampeni ya upandaji miti bilioni 15 na kuchangia katika urejeshaji wa hekta milioni 10.6 za ardhi iliyoharibika kufikia mwaka 2032.

Waziri wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, Dkt. Deborah Barasa, akizungumza jijini Nairobi wakati wa uzinduzi huo, alisema mikakati hiyo si hati za sera pekee bali ni maono na ahadi kwa vizazi vijavyo. Alisisitiza kwamba kampeni ya miti bilioni 15 siyo tu kuhusu kupanda miti, bali pia kuhusu kuponya ardhi iliyoharibika, kurejesha vyanzo vya maji, kujenga ustahimilivu wa tabianchi na kuboresha maisha kupitia kilimo cha misitu. Dkt. Barasa alieleza kwamba Mkakati wa Kilimo cha Misitu, ambao utaongoza hatua kwa miaka kumi ijayo, umejengwa juu ya nguzo kuu zinazojumuisha sera na mifumo ya kisheria, ufadhili na uwekezaji, elimu, utafiti na ubunifu, ukuzaji wa mnyororo wa thamani, hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ujumuishaji wa kijamii.



Salaries & Remuneration Commission



ADVERTISEMENT OF VACANT POSITIONS

Salaries and Remuneration Commission (SRC) is an independent Commission established under Article 230 of the Constitution of Kenya 2010, with the mandate to set and regularly review the Remuneration and Benefits of all State Officers and to advise the National and County Governments on the Remuneration and Benefits of all other Public Officers. In carrying out its mandate, the Commission has to take into account the principles of: fiscal sustainability of the public compensation bill, attraction and retention of requisite skills for service delivery, productivity and performance, transparency, fairness and equity.

The Commission seeks to recruit a qualified and competent person to fill the position of **Head of Human Resources and Administration Level RL3**.

APPLICATION PROCESS

Interested and qualified persons are requested to register and apply to the **SRC E- recruitment Portal**. Details of the position are in the Commission website under Career Section. Hard copies and email applications shall not be considered. Details of the position are in the Commission website.

Upon being successful and granted an offer of employment, the successful candidate **MUST** present and satisfy the requirements of Chapter Six of the Constitution of Kenya 2010 by providing copies of the following documents;

- A valid tax Compliance Certificate from the Kenya Revenue Authority (KRA);
- A valid Certificate of Good Conduct from the Directorate of Criminal Investigation (DCI);
- A valid Clearance Certificate from the Higher Education Loans Board (HELB);
- A valid Clearance Certificate from an approved Credit Reference Bureau (CRB) (Must provide certificate or report); and
- A Valid Clearance form from the Ethics and Anti-corruption Commission (EACC)

Applications to be received on or before **9th October 2025** and only Shortlisted candidates will be contacted.



THE EXECUTIVE OFFICE OF THE PRESIDENT OFFICE OF THE PRIME CABINET SECRETARY AND MINISTRY OF FOREIGN AND DIASPORA AFFAIRS STATE DEPARTMENT FOR NATIONAL GOVERNMENT CO-ORDINATION

PUBLIC NOTICE

CALL FOR PUBLIC PARTICIPATION ON THE DRAFT RELIGIOUS ORGANIZATIONS POLICY, 2024 AND THE DRAFT RELIGIOUS ORGANIZATIONS BILL, 2024

The Presidential Taskforce on the Review of the Legal and Regulatory Framework Governing Religious Organizations in Kenya (the “**Taskforce**”) was constituted vide Kenya Gazette Notice Numbers 5661 of 5th May, 2023 and 6091 of 11th May, 2023. The Taskforce presented its Report to His Excellency the President on 30th July, 2024 and as part of its terms of reference, developed and recommended –

- a) the draft Religious Organizations Policy, 2024; and
- b) the draft Religious Organizations Bill, 2024.

The overall objective of these instruments is to provide a framework for regulation of religious organizations; to combat religious extremism and the abuse of the freedom of religion and connected purposes.

The drafts are available on the Office of the Prime Cabinet Secretary website through the weblink: <https://www.primecs.go.ke/policies-bills-acts>

Following Cabinet's adoption of the Taskforce's Report on 29th July, 2025, the State Department for National Government Co-ordination, which is vested with the mandate of coordinating the implementation of the Taskforce's recommendations, hereby invites the public and all persons likely to be affected by the provisions of the documents above to submit written Memoranda on them. These should reach the undersigned through email address religiousorganizations@primecs.go.ke on or before **22nd October, 2025** using the template provided in the Office of the Prime Cabinet Secretary website through the weblink above.

Hard copies of the written Memoranda may be submitted to the Office of the Principal Secretary, State Department for National Government Co-ordination at the Office of the Prime Cabinet Secretary, Ground Floor, Kenya Railways Building, off Haile Selassie Avenue, Nairobi, and addressed as follows–

Hon. Ahmed Abdisalan Ibrahim
Principal Secretary

State Department for National Government Co-ordination
Kenya Railways Headquarters
P.O Box 30551-00100
Off Haile Selassie Avenue, NAIROBI

Public participation forums shall be announced in due course.

Hon. Ahmed Abdisalan Ibrahim
Principal Secretary
STATE DEPARTMENT FOR NATIONAL GOVERNMENT CO-ORDINATION

Serikali kulinda wavuvi dhidi ya unyanyasaji kutoka mataifa jirani

NA MABEL KEYA –SHIKUKU NA MILTON ONYANGO

Waziri wa Usalama wa Ndani na Utawala wa Kitaifa, Kipchumba Murkomen, amewahakikishia wavuvi wa humu nchini kwamba Serikali itawalinda na kuhakikisha usalama wao katika Ziwa Vic-

toria pamoja na maji ya kimataifa yanayoshirikiwa na nchi jirani. Waziri huyo alibainisha kuwa wavuvi wa Ziwa Victoria mara kwa mara wamekuwa wakikamatwa na kusumbuliwa na maafisa wa usalama kutoka nchi jirani, lakini akawahakikishia Wakenya kwamba hatua maalum zinawekwa ili



Waziri wa Usalama wa Ndani Bw. Onesmus Kipchumba Murkomen akihitubia wanahabari mjini Kisumu wakati wa kongamano la 42 la Jukwaa la Usalama.

kulinda maslahi yao wanapotekeleza shughuli zao za kujipatia riziki. “Tutaongeza nguvu za

doria za walinzi wa pwani kwenye maji yetu, na wakati huohuo tunafanya mashauriano na maji-

rani wetu ili kuhakikisha kwamba usalama katika mipaka ya maji ya kimataifa umeimarishwa kwa manufaa ya raia wa mataifa yote,” alisema. Waziri huyo alitania kwamba samaki hawatambui mipaka iliyowekwa kwenye ziwa, kwani wanaweza kuzaliana katika nchi moja na baadaye kuhamia nchi nyingine, jambo ambalo limekuwa chanzo cha migogoro pale jamii zinapofanya doria kutafuta bidhaa hii muhimu. Alisema doria kwenye maji hayo zitaimarishwa

kwa kutumia boti za kasi za kisasa na kuendeleza ushirikiano na mataifa jirani kama Uganda na Ethiopia, ili kuboresha usalama katika maji ya kimataifa ya nchi. Akihutubia kikao cha 42 cha Jumwa la Usalama kilichofanyika Kisumu, Murkomen alisema kwamba kwa muda mrefu wavuvi wa Kenya wamekuwa wakikamatwa, kuwekwa kizuizini na wakati mwingine kufungwa katika nchi jirani kutokana na ukosefu wa ulinzi madhubuti kwenye maji ya Kenya.



TVET CURRICULUM DEVELOPMENT, ASSESSMENT AND CERTIFICATION COUNCIL (TVET CDACC)

TENDER NOTICE

A. PREQUALIFICATION OF SUPPLIERS AND SERVICE PROVIDERS FOR GOODS, WORKS AND SERVICES FOR THE FINANCIAL YEAR 2025/2026-2026/2027: TENDER NO. CDACC/T/001/2025-2026

TVET Curriculum Development, Assessment and Certification Council (TVET CDACC) intends to pre-qualify and register Suppliers and service providers for the provision of Goods, Works and Services for the financial years 2025/2026-2026/2027.

Interested and competent firms specializing in the provision of goods and services in the categories mentioned here below are invited to apply for pre-qualification/registration.

A. SUPPLY OF GOODS			
S/No	PRE- QUALIFICATION CATEGORY NO.	ITEM DESCRIPTION	ELIGIBLE GROUP
1.	CDACC/PRE/01/2025-2026	Supply and delivery of general stationery items.	AGPO
2.	CDACC/PRE/02/2025-2026	Supply and delivery of desktop computers, laptops, printers, Ipads and related accessories, servers and related accessories, Supply of audio-visual equipment, projectors, projector screens, white board and related items.	Open
3.	CDACC/PRE/03/2025-2026	Supply and delivery of general office equipment, office furniture and fittings	Open
4.	CDACC/PRE/04/2025-2026	Supply and delivery of Mineral Water	AGPO
5.	CDACC/PRE/05/2025-2026	Supply and delivery of Long-life Milk and Beverages	AGPO
6.	CDACC/PRE/06/2025-2026	Supply and delivery of newspapers, magazines, periodicals and publications.	AGPO
7.	CDACC/PRE/07/2025-2026	Supply and delivery of calling cards e.g. Safaricom, Airtel and Telkom scratch cards.	AGPO
8.	CDACC/PRE/08/2025-2026	Supply and delivery of staff uniform, protective gear and clothing.	AGPO
9.	CDACC/PRE/09/2025-2026	Supply and delivery of cleaning materials e.g soaps, detergents and disinfectants.	AGPO
10.	CDACC/PRE/10/2025-2026	Supply and delivery of tyres, tubes and batteries.	Open
11.	CDACC/PRE/11/2025-2026	Supply of Secure papers – Transcript/Certificates	Open
B. PROVISION OF SERVICES			
	CATEGORY NO.	ITEM DESCRIPTION	
12.	CDACC/PRE/12/2025-2026	Provision of printing services e.g brochures, folders, booklets and other promotional materials e.g shirts, caps etc	AGPO
13.	CDACC/PRE/13/2025-2026	Provision of printing services – Occupational Standards, Curriculum, Learning Materials etc	Open
14.	CDACC/PRE/14/2025-2026	Provision of corporate branding, communication and marketing services	Open
15.	CDACC/PRE/15/2025-2026	Provision of travel agency services, air-ticketing and travel arrangements – IATA registered only	Open
16.	CDACC/PRE/16/2025-2026	Provision of engraving and marking of Council Assets	AGPO
17.	CDACC/PRE/17/2025-2026	Provision of Pest control Fumigation Services	AGPO
18.	CDACC/PRE/18/2025-2026	Provision of Events Management	Open
19.	CDACC/PRE/19/2025-2026	Provision of Outside Catering Services	Open

B. PROVISION OF SERVICES			
	CATEGORY NO.	ITEM DESCRIPTION	
20.	CDACC/PRE/20/2025-2026	Provision of Cleaning Services	Open
21.	CDACC/PRE/21/2025-2026	Provision of Security Guard Services	Open
22.	CDACC/PRE/22/2025-2026	Provision of insurance services for Council assets eg motor vehicles	Open
23.	CDACC/PRE/23/2025-2026	Provision of Tracking service to Motor Vehicles.	Open
24.	CDACC/PRE/24/2025-2026	Provision of insurance services medical covers/WIBA	Open
25.	CDACC/PRE/25/2025-2026	Provision of Maintenance services for office equipment eg Computers, Printers, Photocopiers	AGPO
26.	CDACC/PRE/26/2025-2026	Provision of IT security solutions	AGPO
27.	CDACC/PRE/27/2025-2026	Provision of Software designs	Open
28.	CDACC/PRE/28/2025-2026	Provision of repair and maintenance services for motor vehicles (Approved Garages to attach certificate or letter of approval)	Dealers & Approved Garages
29.	CDACC/PRE/29/2025-2026	Provision of motor cycle rider services for short messengerial services	Open
30.	CDACC/PRE/30/2025-2026	Provision of conference facilities	Open
CONSULTANCY SERVICES			
	CATEGORY NO.	ITEM DESCRIPTION	
31.	CDACC/PRE/31/2025-2026	Provision of Consultancy services for Editing of TVET CDACC Documents	Open
32.	CDACC/PRE/32/2025-2026	Provision of Consultancy services for Development of Learning Guides/Materials	Open
33.	CDACC/PRE/33/2025-2026	Provision of Consultancy services for Development of Digital Content	Open
34.	CDACC/PRE/34/2025-2026	Provision of Consultancy services for Recognition of Prior Learning and Related services	Open

The Pre-qualification/Registration of suppliers/contractor(s) documents detailing relevant terms and conditions may be obtained at No cost from the Organization's website www.tvetcdacc.go.ke

Duly completed Pre-qualification/Registration documents in plain sealed envelopes clearly marked with the Tender Number and Pre-qualification Category No. should be mailed or deposited in the Tender Box provided on the 10th floor Absa Towers, Loita Street, addressed to:-

**The Chief Executive Officer,
TVET Curriculum Development, Assessment and Certification Council (TVET CDACC)
P. O. Box 15745-00100,
Nairobi.**

so as to be received on or before **7th October, 2025 at 10:00am East African Time**. Applications/tenders will be opened immediately thereafter at the Board Room on the 10th floor Absa Towers, Loita Street, in the presence of candidates or their representatives who may wish to attend.

Any canvassing in whatever way will render the prospective bidder(s)/applicant(s) ineligible for participation. The Organization reserves the right to accept or reject any application/tender in whole or in part without giving reason(s) for its decision.

COUNCIL SECRETARY/CEO

Kwale, mradi wa KEMFSED wa Sh10b kuimarisha uzalishaji wa samaki

NA HUSSEIN ABDULLAHI NA SHARON NDILA (KNA)

Kaunti ya Pwani ya Kwale, kwa ushirikiano na mradi wa Kenya Marine Fisheries Socio-Economic Development (KEMFSED), imeanzisha miradi inayolenga kuongeza uzalishaji wa samaki, kuboresha usalama wa chakula na kuunda fursa za kiuchumi. Mradi wa KEMFSED wenye thamani ya shilingi bilioni 10 unatekelezwa na Idara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa msaada wa Benki ya Dunia. Mradi huu unaoendesha kuanzia mwaka 2020 hadi 2025 unahusisha kaunti za pwani za Mombasa, Kwale, Kilifi na Lamu, ukiwa na lengo la kuboresha maisha ya jamii za pwani. Mpango huu unaofadhiliwa na wahisani unalenga kupanua upatikanaji wa msaada wa riziki, huduma za usalama wa chakula na ruzuku kwa kaya na biashara masikini na zilizo hatarini, hivyo kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya kaunti za pwani. Kwa kushirikiana na KEMFSED, Kwale imekuwa ikiwezesha wavuvi kwa kusambaza vifaranga vya samaki na pembejeo nyingine za kuendeleza sekta ndogo ya ufugaji wa samaki, huku ikiboresha usalama wa chakula na lishe pamoja na maisha ya wananchi. Kupitia ushirikiano huu, wavuvi wadogo wamepatiwa vifaa kama nyavu za kuvulia za aina ya multifilament, boti za fiberglass zenye injini za nje, masanduku ya baridi, flares, bond liners, vifaa vya GPS, boti za ukoaji na koti za kuokolea—vyote vikiwa na lengo la kugeuza uvuvi kuwa shughuli yenye faida. Vifaa hivyo vya uvuvi vinalenga kuwawezesha na kuongeza uwezo wa wavuvi wadogo katika kaunti ya pwani kuingia kwenye uvuvi wa kina kirefu kwa kiwango kikubwa. Gavana Fatuma Achani anasema ushirikiano huo unalenga kuimarisha uwezo wa wakulima



wa samaki wa eneo hilo kuzalisha zaidi na kuunda fursa za biashara katika ufugaji wa samaki. Gavana Achani anasema usaidizi huo kwa wakulima utawasaidia wavuvi wa eneo la pwani kuziba pengo la uzalishaji wa samaki. Alisema mabwawa ya samaki yatachukua nafasi ya changa-

moto za ukosefu na ugumu wa upatikanaji wa samaki, ambazo zimetajwa kuwa vikwazo katika ufugaji wa samaki eneo hilo. Achani alikuwa akizungumza alipongoza zoezi la kuingiza vifaranga vya samaki 4,000 na chakula cha samaki katika mabwawa mawili ya ufugaji yali-

1. Kutoka kushoto Waziri w Kilimo na Uvuvi wa Kaunti ya Kwale Roman SHERA, Naibu Gavana Fatuma Achani wakifuraha baadhi ya vifaa vya uvuvi vinavyosambazwa kwa wafugaji wa samaki katika Kaunti Ndogo ya Matuga.

2. Samaki wadogo kwenye vidimbwi vya samaki Matuga kaunti ndogo ya Kwale.

yosimamiwa na Matuga Village Elders Self-Help Group katika kijiji cha Dzangadzangani, Kombani, wadi ya Waa/Ngombeni, Kaunti Ndogo ya Matuga. Alisema kikundi hicho kimepewa vifaa vya uzio wa mabwawa, nyavu za kuvulia kwenye mabwawa, vifaa vya baada ya uvunaji, vifaa vya kupima ubora wa maji, vifaa vya sampuli za bwawa, vifaa vya kujikinga na magonjwa na magari za kuhifadhi maji.

Wakulima kufaidika huku Kenya ikizindua sera ya huduma za nyanjani

NA JOSEPH NG'ANG'A

Sekta ya kilimo nchini Kenya inashuhudia mabadiliko ya kimkakati katika namna huduma za ugani na ushauri zinavyotolewa, huku wadau kote nchini wakikusanyika kuunga mkono Sera ya Ugani wa Sekta ya Kilimo (KASEP) ya mwaka 2023. Leonard Kubok, Naibu Mkurugenzi katika Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali za Mazao katika Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, alisema kuwa sera hiyo—iliyotayarishwa kwa ushirikiano kati ya serikali ya kitaifa na za kaunti pamoja na wadau katika utafiti, biashara ya kilimo

na asasi za kiraia—inalenga kuoanisha juhudi, kuboresha utoaji wa huduma, kuimarisha mnyororo wa thamani wa kilimo, na kukuza uhusiano thabiti kati ya utafiti na ugani. Akizungumza wakati wa Mkutano wa 3 wa Kitaifa wa Ugani wa Kilimo ulioandaliwa na Jukwaa la Huduma za Ushauri wa Kilimo-Kenya (KeFAAS), Kubok alibainisha kuwa KASEP 2023 inatoa mfumo wa kitaasisi wa ushirikiano kati ya serikali ya kitaifa na za kaunti katika utoaji wa huduma za ugani wa kilimo. “KASEP inaeleza wazi majukumu ya kila ngazi ya serikali,” Kubok alifafanua. “Serikali ya kitaifa inabaki na jukumu la kutunga



Leonard Kubok, Naibu Mkurugenzi Idara ya Rasilimali za Mazao, Wizara ya Kilimo.

sera na kusimamia utekelezaji wake, huku serikali za kaunti zikihusika na utekelezaji katika maeneo yao. Pia imejumuisha mfumo wa utekelezaji wenye malengo ya muda mfuji, wa kati na wa muda mrefu.” Kwa mujibu wa Kubok, sera hiyo pia inashughulikia masuala muhimu mtambuka kama vile mabadiliko ya tabianchi, ujumuishi, na uthibitishaji wa ubora.



Peter Mwangi, mwakilishi wa KeFAAS.

“Ni lazima tuhakikishe vijana, wanawake, jamii asilia, na wakulima wasio na rasilimali hawabaki nyuma. Ujumuishi ni eneo mahsusi katika sera hii. Pia inaweka viwango vya ithibati kwa watoa huduma za ugani kwa sababu kwa sasa yeyote anaweza kudai kutoa huduma za nyanjani bila sifa za kitaaluma,” alisema Kubok.

WRA yazindua mkakati wa data kupunguza shida ya maji maeneo kame

NA BRIAN MUTUA (MYGOV)

Mamlaka ya Rasilimali za Maji (WRA) imezindua mfululizo wa mikakati ya mageuzi inayolenga kubadilisha kwa kiwango kikubwa namna Kenya inavyokusanya, kuchambua na kutumia takwimu za rasilimali za maji. “Tunahamia kutoka kwenye usimamizi wa maji wa kukabiliana na matukio kwenda katika maamuzi ya utabiri yanayoongozwa na takwimu,” alisema Afisa Mkuu Mtendaji wa WRA, Mohamed Shurie. “Hii inahusu kuhakikisha mahitaji ya maji ya Kenya ya baadaye kwa usahihi na uwajibikaji.” Shurie alibainisha kwamba kiini cha mageuzi haya ni usimikaji wa vituo vya telemetria katika maeneo makuu ya vyanzo vya maji. Kwa mujibu wake, vituo hivi hutoa takwimu za papo kwa papo kuhusu mtiririko wa mito, mvua, na viwango vya maji chini ya ardhi—ambavyo ni muhimu kwa utoaji wa tahadhari za mapema za mafuriko na maandalizi ya ukame. “WRA pia imewekeza katika vifaa vya kijiolojia na vya hidrojiolojia ili kuboresha ramani ya maji ya ardhi, hasa katika maeneo kame na yenye ukame. Teknolojia hii inasaidia kutambua maeneo endelevu ya kuchimba visima na kupunguza changamoto za maji katika jamii zilizo hatarini,” alisema. Ili kuboresha mtandao wake wa ufuatiliaji, Shurie alisema kuwa Mamlaka imeweka mbinu jumishi za kiteknolojia ambazo zinajumuisha ufuatiliaji wa maji ya juu ya ardhi, maji ya chini ya ardhi, ubora wa maji na uchafuzi, pamoja na maabara zilizowekwa rasmi kufanya kazi. “Takwimu za papo kwa papo husaidia katika kufanya maamuzi kuhusu mgao wa rasilimali za maji. Mfumo wa telemetria ukiunganishwa na mita za kisasa unaweza kutoa usawa wa maji wa papo kwa papo na kuongoza katika kuamua viwango,” alisema. “Takwimu zinazokusanywa hukaguliwa, kuchambuliwa na kuhifadhiwa katika Mfumo wa Taarifa za Rasilimali za Maji (WRIS) wa WRA, ambako hupatikana kwa ajili ya matumizi katika upangaji na usanifu wa miradi ya maendeleo ya rasilimali za maji pamoja na utafiti wa kisayansi na kitaaluma,” aliongeza Mkurugenzi huyo. Vivyo hivyo, alifichua kuwa Mamlaka pia imeweka mfumo wa E-permit unaowezesha mgao wa rasilimali za maji kupitia mfumo wa kielektroniki.

Mianzi kuchukua jukumu muhimu kufanikisha azma ya miti 15 bilioni



NA DOMINIC CHERES AND KIBE MBURU

Waziri wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, Dkt. Deborah Barasa, ametangaza kwamba serikali kwa kushirikiana na wadau wa mazingira imepanda miti zaidi ya milioni 900 kote nchini, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais la kupanda miti bilioni 15 kufikia mwaka 2032. Dkt. Barasa, aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Mianzi Duniani 2025 yaliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Kabianga, Kaunti ya Kericho, aliongoza zoezi la upandaji miti ya Mianzi ambapo miche 30,000 ya Mianzi ilipandwa chuoni humo na maeneo jirani. Akizungumza wakati huo, Waziri alisema: “Kwa miaka mingi, uwezo wa Mianzi nchini Kenya ulitambulika lakini haukutumika ipasavyo. Tulijua kwamba Mianzi asilia wa nyanda za juu (Oldenian alpina) ulifunika zaidi ya

hekta 133,000 katika milima ya Aberdare, Mlima Kenya, Mau Complex, Mlima Elgon na safu za Cherangany. Pia tuli leta aina zaidi ya 40 za Mianzi wa kigeni kupitia Taasisi ya Utafiti wa Misitu Kenya (KEFRI), ambapo angalau aina 12 zinastawi vizuri katika maeneo mbalimbali ya kijiografia.” Aidha, Waziri alizindua Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Mianzi 2025-2035, akieleza kwamba sekta ya Mianzi imepiga hatua, ikiwemo kutambuliwa rasmi kiseri baada ya Mianzi kutangazwa kuwa zao la kibiashara mwaka 2020, hatua iliyoweka msingi wa kisheria wa kibiashara. Aliongoza kuwa kampuni kama Pot Enterprises na African Plantation Capital tayari zimeanza mashamba ya Mianzi, huku makundi ya jamii kama Eco Green Kenya yakipanua kilimo. Pia mafundi na biashara ndogo ndogo (SMEs) wameanza kuzalisha samani, kazi za mikono na bidhaa za useremala ku-

tokana na Mianzi, huku KEFRI ikisaidia kwa mafunzo na uhamishaji wa teknolojia. “KEFRI imefanikiwa kuthibitisha aina za Mianzi wa kigeni, na vitalu vya miche kote nchini vinaongeza uzalishaji,” alisema Dkt. Barasa. Waziri pia alibainisha kwamba Kenya inanufaika na ushirikiano kupitia INBAR na Mpango wa Maendeleo ya Mianzi wa Dutch-Sino East Africa, ambao unawaunganisha wakulima na taasisi na wataalamu wa kimataifa pamoja na masoko. Alisema kwamba katika utekelezaji wa Dira ya 2030, Ajenda ya Mageuzi ya Uchumi Kutoka Chini Kwenda Juu (BETA), na agizo la Rais la kufanikisha asilimia 30 ya uoto wa miti kufikia mwaka 2032, Mianzi utachangia moja kwa moja kwenye mpango wa miti bilioni 15. Siku ya Mianzi Duniani, ambayo kaulimbiu yake ilikuwa “Mianzi kwa Watu, Sayari na Suluhu za Tabianchi”, pia il-

1. Waziri wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, Dkt. Deborah Barasa aliongoza wadau wa mazingira katika zoezi la upandaji miti ya mianzi katika Chuo Kikuu cha Kabianga. Kenya ilipoungana na Ulimwengu kuadhimisha Siku ya Mianzi Duniani 2025

2. Waziri wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, Dkt. Deborah Barasa, wakati wa uzinduzi wa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Mianzi ya Kenya 2025 - 2035. Picha na Kibe Mburu

iashiria uzinduzi wa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Mianzi, unaolenga kupanua eneo la Mianzi hadi hekta 150,000 katika misitu, maeneo ya mito na mashambani. Akizungumza kuhusu mkakati huo, Waziri alisema kuwa Mianzi unatarajiwa kuunda ajira za kijani 750,000 katika miaka miwili ya kwanza ya upandaji kupitia mkakati wa kitaifa wa urejeshaji wa mandhari na mi-

fumo ya ikolojia. Pia aliongoza kuwa mradi huo unakusanya Shilingi bilioni 15 kufanikisha kibiashara, minyororo ya thamani na fursa za mikopo ya kaboni. “Tunaliweka Mianzi kama mbadala wa mbao, chanzo mbadala cha karatasi, vifaa vya ujenzi, samani, nguo, nishati na chakula,” aliongoza Waziri. Akihutubia wadau wa mazingira kutoka Chuo Kikuu cha Kabianga, KEFRI, Huduma ya Misitu Kenya na washirika wa misitu binafsi Kericho, Waziri alisema kwamba kupitia mkakati huo, maisha ya watu yataboreshwa, ardhi iliyoharibika itarejeshwa, suluhu za tabianchi zitapatikana na Kenya itajidhihirisha kama kinara wa kikanda katika mnyororo wa thamani wa Mianzi. Kwa upande wake, Mkurugenzi wa KEFRI, Dkt. Jane Njuguna, alisema kwamba nchini Kenya, taasisi hiyo inalea sekta ya Mianzi yenye takribani hekta 140,000 za Mianzi, ambapo hekta 130,000 zina mea kiasili na hekta 10,000 zimepandwa mashambani. Hata hivyo, alisema kuwa shughuli nyingi za Mianzi kwa sasa zinafanyika katika kiwango cha viwanda vidogo vidogo, huku juhudi za viwandani zikiwa zinajitokeza kupitia makampuni kama Green Pots Enterprises na Eco-Pole. Kulingana na Dkt. Njuguna, sekta ya Mianzi inaunga mkono takribani kaya 5,000 kupitia viwanda vidogo na vitalu vya Mianzi vinavyotoka riziki muhimu na kuchochea ukuaji wa uchumi wa ndani. Aidha, alisema utafiti unaendelea ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya Mianzi, ambapo juhudi za sasa zinalenga usimamizi wa vitalu na teknolojia ya tishu, usimamizi wa mashamba na mbinu za uvunaji, usindikaji na tiba ya miti iliyovunwa, kujenga uwezo, kuhamisha teknolojia, kuandaa viwango na kuongeza uelewa kupitia maonyesho ya kibiashara na juhudi nyinginezo.

MAKALA MAALUMU: USALAMA WA CHAKULA

Wakulima wa Tindiret wageukia ndizi kwa mavuno ya mwaka mzima

NA SAMMY MWIBANDA (KNA)

Kilimo cha ndizi kinajitokeza kwa kasi kama moja ya vyanzo vya kuaminika vya mapato kwa kaya katika Tarafa Ndogo ya Tindiret, ambako wakulima wamekumbatia zao hilo kama chakula cha msingi na pia kama biashara. Wakulima kote Tindiret wanageukia ndizi kwa sababu ya kustahimili changamoto za hali ya hewa na pia kutokana na mahitaji makubwa sokoni. Mkulima wa eneo hilo, Joseph Kiptoo kutoka Kijiji cha Kapkoros, anasema aligeukia kilimo cha ndizi

miaka mitano iliyopita baada ya mavuno ya mahindi yasiyotabirika kumwacha aki-hangaika kulisha familia yake. “Ndizi ni za kuaminika zaidi,” alieleza, akibainisha kuwa ndizi hutoa mavuno kwa mwaka mzima, tofauti na mahindi ambayo hupandwa mara moja tu kwa mwaka. Mkulima mwingine, Mary Jepchumba kutoka Chepsangor, alisema ndizi zimebadilisha maisha yake. Hapo awali alipanda ekari moja pekee, lakini sasa amepanua hadi ekari tatu, akipata mapato ya kutosha kusomesha watoto wake na kujenga nyumba ya kudumu. “Mapato ni ya uhakika, na daima kuna mnunuzi, iwe ni



wa hapa nyumbani au katika masoko ya jirani,” alisema. Kulingana na Afisa wa Kilimo wa Tarafa Ndogo ya Tindiret, Peter Sang, kilimo cha ndizi kimekuwa nguzo ya usalama wa chakula katika eneo hilo. Alibainisha kuwa zaidi ya wakulima 600 wameanza kulima ndizi katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita,

Shamba la migomba. Wakulima wa Tindiret wamekumbatia zao hilo kwa madhumuni ya msingi na kibiashara.

wakihimizwa na huduma za ugani za kaunti. “Tunapigia debe ndizi zilizozaishwa kwa teknolojia ya tissue culture ambazo hustahimili magonjwa na kutoa mavuno mengi zaidi,” alieleza.

Kwa kaya nyingi, mabadiliko haya yameenda mbali zaidi ya kipato na kugusa lishe. Familia kama ile ya Samson Chebet huko Songhor hutegemea ndizi kwa mlo wa kila siku, na hivyo kupunguza utegemezi wa unga wa mahindi. Maafisa wa lishe wa kaunti pia wamesifu ndizi kama chanzo bora cha vitamini na nyuzinyuzi, muhimu katika kupambana na utapiamlo vijijini. Athari za kifedha zimekuwa kubwa. Wafanyabiashara na madalali kutoka Eldoret na Kisumu hukimbilia masoko ya Tindiret kununua ndizi kwa wingi. Janet Cheruiyot, mkulima kutoka Tindiret Centre, alisema hupata zaidi ya shilingi 30,000 kila mwezi kutokana na mauzo ya ndizi, pesa zinazosaidia familia yake na pia kuendeleza mradi wake mdogo wa maziwa.

Rais Ruto azindua Vipingo SEZ ya ekari 2,000 kuendeleza kazi, uwekezaji na ukuaji viwanda

NA VICTORIA NJERI (PCO)

Rais William Ruto amezindua mradi wa ujenzi wa awali wa Eneo Maalum la Kiuchumi (SEZ) la Vipingo lenye ukubwa wa ekari 2,000 katika Kaunti ya Kilifi, ikiwa ni kilele cha siku ya pili ya Jukwaa la Uwekezaji la Arise Integrated Industrial Platforms (IIP) – Kenya 2025. Mradi huu, ambao ni wa kimkakati chini ya kaulimbiu “Kufungua Fursa Kupitia Maeneo Maalum ya Kiuchumi,” unalenga kuharakisha kazi ya viwanda nchini Kenya kwa kuongeza thamani ya mazao, kuunda maelfu ya nafasi za kazi na kuifanya Kenya kuwa kitovu cha kimataifa cha uzalishaji endelevu. SEZ ya Vipingo ni ushirikiano kati ya Arise IIP, Centum, Afreximbank, Africa Finance Corporation (AFC) na Vision Invest. Mradi iliyopangwa ni pamoja na kiwanda cha nguo kitakachotoa ajira kwa watu 30,000 na kiwanda cha kuunganisha pikipiki za kielektroniki na za umeme. Kupitia kupunguza utegemezi wa mauzo ya malighafi ghafi, SEZ inalenga kuongeza ajira, kuimarisha minyororo ya usambazaji na kuongeza ushindani wa Kenya katika masoko ya kikanda na ya kimataifa. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Rais Ruto alisisitiza umuhimu wa kuongeza thamani ya mazao nchini. “Eneo Huru la Biashara Barani Afrika siyo tu makubaliano ya kibiashara; ni dira ya bara la soko moja lenye watu bilioni 1.4. Ili Afrika inufaike, ni lazima tuache kuuza malighafi na badala yake tuongeze



Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda, Lee Kinyanjui (Katikati), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji nchini Bw. John Mwendwa (kulia kwake), Wang Feng (kushoto kwake) na Rais William Ruto, wakati wa kutia saini rasmi makubaliano na kampuni ya China ya Shandong Linglong Tyre ya kuanzisha kiwanda cha kutengeneza matairi cha dola milioni 800 katika eneo Maalum la Kiuchumi Mombasa, Kaunti Kisiwani Mombasa.

thamani hapa nyumbani.” “Uzinduzi wa SEZ ya Vipingo ni mwanzo wa enzi mpya – sura ya ajira kwa vijana wetu, fursa kwa biashara zetu, teknolojia kwa viwanda vyetu na ustawi kwa wananchi wetu,” alisema. Kiongozi wa Taifa pia aliwahakikishia wawekezaji dhamira ya Kenya katika sera thabiti, usalama wa nishati na ukuaji wa miundombinu. Alifichua kuwa serikali imewekeza dola milioni 50 katika SEZ hiyo, inalenga kuzalisha megawati 10,000 za umeme ifikapo 2027 na inaendelea kujenga miun-

dombinu ikiwemo barabara kuu ya Mombasa–Malindi na upanuzi wa reli hadi Uganda. Taasisi za kifedha ziliahidhi msaada mkubwa kwa mradi huo. Rais wa Afreximbank, Prof. Benedict Oramah, alitangaza kuanzishwa kwa kituo cha majaribio ili kupunguza muda wa usafirishaji wa bidhaa, huku KCB Group PLC na Benki ya Afreximbank wakitia saini makubaliano ya kusaidia wawekezaji katika SEZ ya Vipingo. Chini ya makubaliano hayo, Afreximbank itatoa ufadhili

wa awali wa dola milioni 500 za Marekani na KCB Group dola milioni 300 za Marekani ili kuwezesha msaada wa kifedha na kibiashara kwa wawekezaji watarajiwa. “Mfumo wetu wa pamoja utawawezesha wawekezaji wa ndani na wa kimataifa kupata suluhu za kifedha zenye ushindani, zikiwemo mikopo ya miradi, vifaa vya biashara na msaada wa ushauri,” washirika hao walisema kwa taarifa ya pamoja. Pembeni mwa jukwaa hilo, Kenya ilisaini makubaliano ya

